THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

**MINISTRY OF WATER**

**NATIONAL WATER FUND**

# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA KITENGO CHA UHAKIKI WA MIRADI NA UTAFUTAJI WA RASILIMALI

## ROBO YA NNE YA MWAKA 2023/2024

## 1. UTANGULIZI

Kwa mujibu wa Muundo wa Taasisi ya Mfuko wa Taifa wa Maji ulioidhinishwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kitengo cha Uhakiki wa Miradi na Utafutaji wa Rasilimali kinaundwa na sehemu pili (2) ya muundo huo. Aidha kitengo kina sehemu mbili chini yake ambazo ni Sehemu ya Uhakiki wa Miradi na Huduma za Kiufundi pamoja na Sehemu ya Utafutaji wa Rasilimali.

## 2. KAZI ZILIZOTEKELEZWA KATIKA SEHEMU YA UHAKIKI WA MIRADI NA UTAFUTAJI WA RASILIMALI

| Na | Kazi | Utekelezaji |
|---|---|---|
| 1 | Kuandaa vigezo na utaratibu wa utoaji wa fedha kwa watekelezaji wa miradi ya maji | Tulizielekeza taasisi zinazotekeleza miradi ya maji na kusimamia uzingatiaji wa vigezo vya upangaji wa miradi itakayotekelezwa katika bajeti yam waka 2024/2025 kwa kuzingatia miongozo na maelekezo ya Bodi ikiwemo;<br>i) Kuhakikisha kipaumbele kinawekwa kwenye miradi inayoendelea,<br>ii) Kuwa na miradi mikubwa ya kimkakati itakayofadhiliwa na Mfuko hadi kukamilika,<br>iii) Kubainisha na kutenganisha miradi yenye ufadhili zaidi ya mmoja ili kuzuia malipo mara mbili,<br>iv) Miradi kuendana na vipaumbele vya sekta ya maji. |
| 2 | Kuhakiki miradi kulingana na vigezo vya kihandisi | Kazi hii imetekelezwa sambamba na Kazi Na. 1 hapo juu. |
| 3 | Kuandaa nyenzo za utekelezaji ikiwemo fomu na miongozo itakayotumika wakati wa uwasilishaji wa maombi na kuidhinisha malipo ya fedha kwenye miradi ya maji | Tuliboresha fomu ya vigezo vya uwasilishaji wa madai ya fedha kwa miradi inayotekelezwa na Wakandarasi au kwa utaratibu wa wataalam wa ndani (force account). Fomu hiyo imekuwa kiambatisho cha mwongozo wa utoaji wa fedha. |
| 4 | Kutathmini maombi ya fedha na kupendekeza malipo ya miradi kwa Bodi | Katika kipindi cha robo ya nne tumehakiki na kuidhinisha malipo ya miradi 61 yenye jumla ya shilingi 15,090,000,000. Kati ya miradi hiyo jumla ya miradi 30 yenye kiasi cha shilingi 7,369,329,898.30 ni ya vijijini; miradi 23 yenye kiasi cha shilingi 4,366,643,985.20 ni ya mijini na miradi 8 yenye kiasi |

| | | |
|---|---|---|
| | | cha shilingi 893,336,759 ni ya utunzaji wa vyanzo vya maji. |
| 5 | Kusimamia mfumo wa taarifa za miradi iliyoidhinishwa, inayoendelea kutekelezwa na iliyokamilika | Tumeendelea kuhuisha kanzidata ya miradi inayoonesha taarifa za miradi yote iliyopokea fedha za mfuko na hali ya utekelezaji wake. Jumla ya miradi 2,305 yenye kiasi cha shilingi 891,269,839,968.91 imetekelezwa kati ya mwaka 2015/2016 Mfuko ulipoanzishwa hadi sasa. Kati ya miradi hiyo jumla ya miradi 1524 yenye kiasi cha shilingi 518,435,508,483.61 ni ya vijijini, miradi 612 yenye kiasi cha shilingi 330,408,385,449.67 ni ya mijini na miradi 169 yenye kiasi cha shilingi 42,425,946,035.63 ni ya utunzaji wa vyanzo vya maji |
| 6 | Kuandaa viashiria vya utekelezaji wa miradi kwa ajili ya kuzingatiwa na watekelezaji wa miradi na kutunza taarifa za miradi | Tumehuisha viashiria vya utekelezaji kwa ajili ya kupima watekelezaji wa miradi ya maji katika bajeti ya mwaka 2024/2025 |
| 7 | Kujenga uwezo kwa taasisi zinazotekeleza miradi ya maji | Tumeendelea kujenga uwezo kwa taasisi zinazotekeleza miradi ya maji ikiwemo kuwaelekeza utaratibu na vigezo vya uombaji wa mkopo wa fedha za Mfuko. mwezi juni, 2024 wataalam wawili (Mhandisi na Mhasibu) walikwenda katika Mamlaka ya Maji Mwanza kusaidia ukamilishaji wa nyaraka za kuomba mkopo ambapo maombi ya kiasi cha shilingi 8,046,119,805 tayari yamewasilishwa TIB. Uchambuzi wa maombi hayo unaendelea. |
| 8 | Kuandaa na kutekeleza mkakati wa utafutaji wa rasilimali | i) Tulifanya kikao na taasisi ya Water.ORG kwa ajili ya kujadili hati ya makubaliano (MoU) kwa ajili ya kusaidia kujenga uwezo kwa mamlaka za maji katika uandaaji wa maandiko na kusaidia Mfuko katika utafutaji wa rasilimali.<br><br>ii) Tumekamilisha maandiko ya miradi Matano kutoka katika Mamlaka za Maji za Mafinga, Makambako, Mbeya, Morogoro na Mwanza. |

| | | |
|---|---|---|
| | | iii) Tumeendelea kushirikiana na USAID/MUM kukamilisha taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri wa kusaidia Mamlaka za Maji kubainisha maeneo ya miradi na kuandaa maandiko ya miradi. |
| 9 | Kuratibu utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa watekelezaji wa miradi ya maji | i) Tumeendelea kuratibu maombi ya mikopo na utoaji wa fedha ambapo jumla ya Mamlaka za Maji 18 zimeshawasilisha maombi ya mkopo yenye jumla ya shilingi Bilioni 23.96. Kati ya maombi hayo tayari mkopo wa shilingi bilioni 5.3 umeshatolewa kwa mamlaka tatu za Bunda (Shilingi milioni 800); Tanga (Shilingi bilioni 1.5) na DAWASA shilingi bilioni 3.<br>ii) Katika kipindi cha robo ya nne tumepokea marejesho ya riba ya mkopo kiasi cha shilingi milioni 12 kutoka Mamlaka ya Maji Bunda. |